# KIDOLE CHA MUNGU

Siku moja nilimtembelea rafiki yangu wa Kiafrika katika nyumba  yake iliyopewa jina "Kidole cha Mungu". Niliambiwa kuwa jirani kadhaa walichukia jina hilo hata wakawashutumu wenye nyumba hiyo kwa kosa la kukufuru, huku wakitisha kupaangamiza mahali pale.

Jambo hili lilinifanya nitafakari swali hili: Je, kweli ni kukufuru kufikiri au kuongea kuhusu kidole cha Mungu? Kabla hatujaamua, hebu tuangalie mistari kadhaa katika Biblia inayoeleza habari za kidole cha Mungu.

## Tukio la Kutisha

Katika kitabu cha Danieli tunaona tukio la kutisha kabisa wakati Mfalme wa Uajemi, Bel- shaza, alipokuwa akila na kunywa kupita kiasi pamoja na wakuu wake. Akiwa amelewa kabisa kwa ajili ya ukuu wake, aliamuru vyombo vya dhahabu vya hekalu la Mungu la Yerusalemu viletwe karamuni ili yeye na wenzake wapate kuvinywea. Kwa Ghafla mkono ukaonekana ukutani na kidole kika- andika kwa herufi kubwa maneno yasiyoeleweka: *"Mene, Mene, Tekeli na Peresi"*. Kidole cha Mungu kimetoa hukumu juu ya mfalme na wafuasi wake waliofanya upuzi: *"Umepimwa katika mizani nawe umeonekana kuwa umepunguka"* (Danieli 5:27).

Ujumbe huu ulimtisha sana yule mfalme mwenye kiburi aliyeishi maisha ya kila aina ya anasa. Kidole cha Mungu kilipoandika ule ujumbe ukutani, mfalme huyo alikuwa kama tayari amekufa - kwani hakumaliza muda wa masaa 24 kabla hajauawa.

## Onyo Kali

Lakini hebu tujifikirie sisi. Kidole cha Mungu kimekuwa kikituandikia sote mapenzi yake juu yetu, tuwe “wakubwa” au "wadogo". Mungu alipompa nabii Musa sheria yake takatifu kwenya Mlima Sinai, alichonga Amri Kumi kwenye mawe mawili akitumia chanda (kidole) chake Mwenyewe (taz. Kutoka 31:18). Kanuni zilizotolewa katika amri hizo ndizo msingi wa sheria za mataifa mengi duniani. Kila mgeni anapaswa kujifahamisha sheria za nchi anayotembelea ili ajiepushe na adhabu.

Vile vile Mungu anatarajia tutii amri zake. Kuwa kwenye hukumu ya mwisho ya Mungu na kujikuta mwenye hatia na kupewa adhabu ni vibaya sana kuliko hukumu yoyote ya kibinadamu. Bwana Yesu alieleza wazi alipowaonya waliomsikiliza: *"Nami nawaambia ninyi rafiki zangu, msiwaogope hao wauuao mwili, kisha baada ya hayo hawana wawezalo kutenda zaidi. Lakini nitawaonya mtakayemwogopa; mwogopeni yule ambaye akiisha kumwua mtu ana uweza wa kutupa katika Jehanum; naam, nawaambia, Mwogopeni huyo."* (Luka 12:4-5). Vile vile katika Waebrania 10:31 tunaonywa: *Ni jambo la kutisha kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai."*

Tulipokuwa watoto tulijua kuwa pengine tusingeadhibiwa makosa ya kutotii au adabu mbaya kiasi fulani. Lakini tulipovuka mpaka na kumkasirisha baba yetu kupita kiasi, kidole chake cha shahada kiliamshwa, ishara hiyo ilikuwa onyo ya mwisho, nasi tulifahamu: hatua moja  zaidi tunajikuta taabuni. Kama tuliendelea, tuliadhibiwa vikali kweli.

# Ujumbe Mzito

Ninakumbuka pia wale waganga wa mfalme Farao wakati wa Musa. Walitambua maonyo ya Mungu katika misiba waliyoipata. Walipokubali kuwa hawangeweza kuendelea kudhihaki hukumu ya Mungu kwa kuiga ishara Zake, walitamka wazi *"Jambo hili ni chanda cha Mungu"* (Kutoka 8:19). Walimwambia mfalme wao: Usipoitikia onyo hili la Mungu wa Musa, utalipa gharama kubwa. Na kweli alilipizwa uhai wa mtoto wake wa kwanza kwa sababu ya kutotii kwake.

**Rafiki mpendwa, usidhihaki kidole cha Mungu anapoongea nawe. Hili si jambo la kuchukuliwa kimchezo, ni jambo la kufa na kupona.**

## Uongozi Dhahiri

Kuna matumizi mengine ya kidole chetu katika kutoa ujumbe. Tunapofuata njia fulani mara ya kwanza kabisa, huenda tukafika njia panda ambapo hatujui tuende wapi. Bila shaka sisi hushukuru sana kumwona mtu ajuaye njia awezaye kutuelekeza kwa kutumia kidole chake.

Sisi sote ni wageni kwenye njia ya maisha. Kila mmoja wetu anakwenda safari hii mara moja tu. Hata kama tuna elimu ya juu, mali nyingi au cheo cha juu kidini, mara kwa mara tunajisikia tumechanganyikiwa na kukata tamaa. Je, hutamani kuwa na mtu wa kukuongoza njiani? Je, hutaki kuwa na uhakika wa kukubaliwa na Mungu, upate kukaa pamoja na yeye milele?

## Kusamehewa

Mwanamke fulani alipatikana akizini akaletwa mbele za Yesu. Viongozi wa kidini walidai ahukumiwe na kupewa adhabu ya sheria ya Musa. Tunasoma katika Injili ya Yohana, sura ya nane, jinsi walivyomzunguka Yesu na kumshurutisha atoe hukumu yake. Lakini walishangaa Yesu alipoinama na kuanza kuandika kwenye mchanga na kidole chake. Sisi sote tungependa kujua aliandika nini, lakini tunajua tu yale aliyowaambia wale viongozi wa Wayahudi waliomzunguka: *"Yeye asiye na dhambi miongoni mwenu na awe wa kwanza wa kumtupia jiwe."*

Hapakuwa na mkono hata mmoja uliookota jiwe. Badala yake, kila mmoja wao aliondoka, wazee halafu vijana, wakiwa wamehukumiwa mioyoni mwao juu ya dhambi zao wenyewe."*Yesu akajiinua asimwone mtu ila yule mwanamke, akamwambia, Mwanamke, wako wapi wale washitaki wako? Hakuna aliyekuhukumu kuwa na hatia? Akamwambia, Hakuna, Bwana, Yesu akamwambia, Wala mimi sikuhukumu. Enenda zako; wala usitende dhambi tena."*

Mtu fulani amesema:

**“Mungu huandika sheria zake kwenye miamba, lakini huandika moyo wake kwenye mchanga.”**

*Rafiki mpendwa, hatuwezi kamwe kugeuza kanuni na sheria za Mungu kufuatana na mapenzi yetu. Sisi sote tunastahili hukumu tunapolinganisha maisha yetu, maneno na matendo yetu na kanuni ya haki na utakatifu iliyowekwa na Hakimu wa Wanadamu. Lakini ni kweli pia kwamba Mungu kutokana na upendo wake kwa ajili ya mwenye dhambi ameonyesha njia ya kurudi katika ushirikiano pamoja na yeye kutokana na upendo mkuu uliodhihirishwa katika maisha ya Yesu Masihi na kifo chake. Huenda tusipende wazo hili, lakini je, ni nani awezaye kuthubutu kupinga uchaguzi wa kifalme wa Mungu:* ***Yesu ndiye abebaye dhambi zetu!*** *Yeye ataka tukubali maneno yake tupate uzima kabla hatujachelewa, na kukabiliwa na kidole cha Mungu cha hukumu ambacho hakiepukiki kamwe.*

*Je, waonaje: Ni kukufuru kujikumbusha mwenyewe pamoja na kuwakumbusha wengine kuhusu kidole cha Mungu? Karibu utushirikishe maoni yako kuhusu andiko hili.*

***(Walter Eric)***